*BUSEGA DC JARIDA*

**Toleo Na. 2**

**JULAI, 2021**

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# OFISI YA RAIS
# TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
# HALMASHAURI YA WILAYA YA BUSEGA




TOLEO LA ROBO YA NNE 2020/2021



**Linatolewa Na Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Busega, S.L.P 157**

Toleo Na. 2

www.busegadc.go.tz
@busegadc
busegadc
@busegadistrict
halmashauri ya wilaya ya busega

## YALIYOMO

**UTANGULIZI** ..................................................... 1

**Lengo la Jarida**............................................... 1

Busega kuongeza Thamani Zao la Pamba……….2

Uzinduzi Msimu waUnunuzi wa Pmaba Kitaifa 2021/2022 Wafanyika Busega………………………4

Baraza la Madiwani Busega Lataka Uwepo wa Mahamaka ya Wilaya……………………………………5

Ziara ya Kamati ya Siasa Wilaya ya Busega yatembelea Miradi ya Maendeleo……………….6

RC David Kafulila Ataka Uvuvi kuwa Kichocheo cha Maendeleo Busega……………………………………..9

Mbio Maalum za Mwenge wa Uhuru Wilayani Busega………………………………………………………10

Ziara ya Mkuu wa Mkoa wa Simiyu Mhe. David Kafulila, Busega………………………………………13

Busega yang'ara UMITASHUMTA, UMISETA Ngazi ya Mkoa………………………………………………………15

## UTANGULIZI

*Halmashauri ya Wilaya ya Busega ni mojawapo ya Halmashauri 6 zilizopo Mkoa wa Simiyu. Halmashauri ya Wilaya ya Busega imeanzishwa mwaka 2013 ikiwa ina Tarafa 2, Kata 15, Vijiji 59 na Vitongoji 362. Halmashauri ya Wilaya ya Busega ina jumla ya Madiwani 20 ambapo madiwani 15 ni wa kuchaguliwa na Madiwani 5 ni wa viti maalum.*

*Kijiografia wilaya ya Busega inapakana na Wilaya ya Magu upande wa Magharibi, Wilaya ya Ukerewe upande wa kaskazini, Wilaya ya Bunda upande wa mashariki na kwa upande wa kusini imepakana na Wilaya ya Bariadi na Itilima. Wilaya ya Busega ina jumla ya ukubwa wa Kilometa za mraba 2129, ambapo Kilometa za mraba 1524 ni nchi kavu, na Kilometa za mraba 605 ni sehemu ya maji (Ziwa Viktoria).*

## LENGO LA JARIDA

Busega DC Jarida linalenga kuhabarisha na kuelezea shughuli za matukio mbalimbali ya Kiserikali Wilayani Busega, shughuli za utekelezaji wa Miradi na Matukio mengine muhimu Wilayani Busega. Pia Jarida hili linalenga kupanua wigo wa wakazi wa Busega na walio nje ya Busega kupata Habari na taarifa mbalimbali za shughuli za maendeleo zinazotekelezwa Wilayani humo. Jarida hili huandaliwa na Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Busega. Toleo la Jarida hili huchapishwa kila baada ya Miezi Mitatu. Pia kupata taarifa, matangazo na miongozo mbalimbali unaweza kutembelea Tovuti ya Halmashauri: www.busegadc.go.tz na Mitandao ya Kijamii Instagram: Busega_Dc; Facebook: Halmashauri ya Wilaya ya Busega na YouTube Channel: BusegaDc

## Busega Kuongeza Thamani ya Zao la Pamba; Maafisa Ugani Wapewa Mafunzo ya Uzalishaji Wenye Tija wa Zao la Pamba

Wakulima Wilayani Busega wametakiwa kuongeza thamani ya zao la Pamba kwa kufuata njia bora za kilimo na njia bora za uchakataji pamba kwa kutumia mashine. Hayo yamesemawa na Mkurugenzi Mtendaji halmashauri ya Wilaya ya Busega Bw. Anderson Kabuko wakati wa mafunzo ya kilimo cha pamba yaliyofanyika katika kituo cha utafiti wa kilimo Ukiriguru mkoani Mwanza. Katika mafunzo hayo yaliyofanyika kuanzia tarehe 26 hadi 30 Aprili, 2021 yamehusisha maafisa ugani na wadau wa kilimo kutoka Wilayani Busega.



Picha ya pamoja Wakufunzi kutoka Chuo cha Utafiti wa Kilimo na Washiriki wa Mafunzo ya Kilimo cha Pamba kutoka Wilayani Busega, wakiongozwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Busega, Bw. Anderson Kabuko.

Picha: Maafisa Ugani kutoka Wilaya ya Busega wakiwa kwenye Mafunzo ya Uzalishaji wa Zao la Pamba katika Chuo cha Utafiti wa Kilimo Ukiriguru Mkoani Mwanza.



www.busegadc.go.tz
@busegadc busegadc
@busegadistrict halmashauri ya wilaya ya busega



**Picha: Washiriki wa Mafunzo ya Kilimo cha Pamba kutoka Wilaya ya Busega wakiwa katika Shamba la mfano katika Kituo cha Utafiti wa Kilimo Ukiriguru Mkoani Mwanza.**

"Tunataka kufanya mapinduzi ya kilimo cha pamba kwa kuongeza uzalishaji wa kilimo hicho Wilayani Busega, baada ya mafunzo haya tutapita katika kata zetu kutoa elimu ya uzalishaji wa kilimo cha pamba" alisema Kabuko. Katika mafunzo hayo miongoni mwa elimu muhimu waliyoipata washiriki ni pamoja na uongezaji wa thamani wa zao la pamba.

Kwa upande mwingine, Bw. Kabuko amesema licha ya dhamira ya Wilaya kuboresha uzalishaji wa zao la pamba kwa kuongeza uzalishaji, suala la thamani ni kipaumbele katika kulinda maslahi ya mkulima na hivyo halitachukua muda mrefu katika utekelezaji wake. "Ni vyema kuongeza thamani ya pamba, hivyo tunadhamiria kuanza na mashine kwa baadhi ya maeneo machache na baadae kununua mashine za kutosha" aliongeza Kabuko.



**Picha: Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Busega, Bw. Anderson Kabuko, akiwa na washiriki wengine katika Shamba la mfano katika Kituo cha Utafiti wa Kilimo Ukiriguru Mkoani Mwanza.**

Awali, Kaimu Mkurugenzi kituo cha utafiti wa kilimo Ukiriguru Dkt. Henerico Kulembeka, amesema ili kuboresha zao la pamba ni muhimu zao hilo liwe na manufaa kwa wakulima, hivyo ni muhimu kutumia mashine katika uchakataji ili kuongeza thamani ya pamba kwa kupata pamba nyuzi, mbegu, mafuta na mashudu ambayo hutumika kama chakula cha mifugo.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa halmashauri ya Wilaya ya Busega Mhe. Sundi Muniwe, amewataka maafisa ugani kutumia elimu waliyoipata kuongeza uzalishaji wa zao la pamba ili Wilaya ya Busega iwe mfano wa kuigwa. Pia Mhe. Muniwe amesema ili kuleta ufanisi wa dhumuni la mafunzo hayo ni vyema kushirikiana na vyama vya ushirika na kuhamasisha matumizi ya mashine ya kuchakata pamba ili kutenganisha pamba nyuzi, mbegu, mafuta na mashudu kwa lengo la kuongeza thamani. "Tumekuja kujifunza, na tunaamini tumepata kitu kikubwa na tutafanya mapinduzi makubwa katika kilimo cha pamba katika Wilaya ya Busega" alisema Mhe. Muniwe.

www.busegadc.go.tz
@busegadc busegadc
@busegadistrict halmashauri ya wilaya ya busega

Zao la pamba Wilayani Busega ni miongoni mwa mazao ya biashara yanayolimwa na wakulima wengi Wilayani Busega, lakini uzalishaji wake ni mdogo kwani kwa ekari 1 kwasasa huzalisha kilogramu 175 hadi 200. Hivyo, lengo la mafunzo ni kuhakikisha uzalishaji wa pamba unapanda kutoka msimu mmoja hadi mwingine. Ili kuongeza uzalishaji Bw. Kabuko amesema malengo ya Wilaya ni kuzalisha wastani wa kilogramu 1,200 kufikia mwaka 2024/2025.

Katika mafunzo hayo washiriki wameweza kupata elimu ya kanuni bora za kilimo cha pamba, njia ya kisasa ya uzalishaji wa mbegu za pamba, udhibiti wa magonjwa shambulizi kwa zao la pamba, matumizi ya bora ya mbolea elekezi na uongezaji wa thamani ya pamba. Wadau walioshiriki mafunzo hayo wamesema elimu waliyoipata ina manufaa makubwa katika kilimo cha pamba, hivyo wameomba utekelezaji ufanyike ili kupata matokeo yaliyokusudiwa. Kwa upande wao maafisa ugani, wamekiri kwamba licha ya changamoto zilizopo kweye kilimo cha pamba, lakini kwa kupitia mafunzo hayo wanaamini watafanyike kile kinachokusudiwa ili kuleta mapinduzi makubwa kwenye kilimo cha pamba Wilayani Busega.

## Uzinduzi Msimu wa Ununuzi wa Pamba Kitaifa 2021/2022 Wafanyika Busega; Wadau Watakiwa Kushirikiana Ili Kuongeza Tija ya Zao la Pamba

Msimu wa ununuzi wa Pamba kitaifa 2021/2022 umezinduliwa wilayani Busega, mkoani simiyu. Akizindua, msimu wa ununuzi wa pamba, Mkuu wa Wilaya ya Busega Mhe. Tano Mwera kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, Mhe. Mwera amesema ushirikiano wa wadau wa kilimo cha pamba utaongeza tija ya zao hilo.



Pichani ni Aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Busega Mhe. Tano Mwera (katikati), Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Busega Mhe. Sundi Muniwe (wa kwanza kulia) na Mkurugenzi wa bodi ya pamba, Bw. Marko Mtunga.

“Zao la pamba ni miongoni mwa mazao ya kimkakati, hivyo wadau washirikiane ili kuongeza tija”, alisema Mhe. Mwera. Katika kuleta tija ni vyema wakulima kufuata kanuni za kilimo bora ikiwemo upandaji wa pamba kwa nafasi inayotakiwa ili kuongeza uzalishaji wa zao hilo, aliongeza Mhe. Mwera.

Awali, Mkurugenzi wa bodi ya pamba, Bw. Marko Mtunga amesema uzinduzi wa msimu wa ununuzi wa pamba una manufaa makubwa hivyo Busega imepewa heshima kubwa, na hii imetokana na kazi kubwa ya usimamizi mzuri wa viongozi wa Wilaya katika kilimo cha pamba. “Katika msimu wa 2020/2021, wilaya ya Busega imezalisha takribani kilo milioni 3, lakini msimu wa mwaka 2021/2022 tunategemea uzalishaji zaidi ya kilo milioni 10” aliongeza, Mtunga.

Aidha, Mhe. Mwera amesema licha ya Wilaya kuwa na uzalishaji mzuri katika zao la pamba,

www.busegadc.go.tz
@busegadc
@busegadistrict
busegadc
halmashauri ya wilaya ya busega

lakini changamoto kubwa inayowakabili wakulima, ikiwemo wadudu. Hali hiyo imewafanya wakulima wengi kushindwa kutambua jinsi ya kukabiliana na wadudu wanaoshambulia zao la pamba, hivyo bodi ya pamba itoa elimu zaidi kwa wakulima ikiwemo elimu ya kupambana na wadudu.

Kauli mbiu ya uzinduzi wa msimu ununuzi wa pamba kitaifa 2021/2022 inasema "**Tuboreshe Ubora na Usafi wa Pamba kwa Uhakika wa Soko na Malipo kwa Wakati".** Kauli ambayo imeelezwa kuwa na manufaa makubwa kwa wakulima wa zao la pamba. Wanunuzi wa pamba walioshiriki uzinduzi huo wamesema wapo tayari kununua pamba na kuahidi wakulima watalipwa kwa wakati. Katika uzinduzi huo, Serikali imetoa bei elekezi ya zao la pamba kwa msimu wa 2021/2022, ambapo pamba daraja A itanunuliwa kwa Tzs 1,050 na daraja B itanunuliwa kwa Tzs 525.

Baadhi ya wa wakulima wa pamba Wilayani Busega wanasema Serikali, wakulima na wadau wengine wanapaswa kushirikiana ili kuongeza uzalishaji wa zao la pamba nchini. Kwa upande mwingine wameiomba Serikali kutoa elimu zaidi ya zao hilo ikiwemo kanuni bora za ulimaji wa zao hilo.

## Baraza La Madiwani Busega Lataka Uwepo wa Mahakama ya Wilaya; Lashauri Marekebisho Stendi ya Wilaya; Lahoji Uwezo wa TEMESA



**Picha: Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Busega Mhe. Sundi Muniwe wakati wa Kikao cha Baraza la Madiwani Robo ya Tatu.**

Baraza la madiwani halmashauri ya Wilaya ya Busega limetaka uwepo wa Mahakama ya Wilaya Busega. Hayo yamesemwa na wajumbe wa baraza hilo wakati wa kikao cha baraza la madiwani robo ya tatu lililofanyika leo 04 Juni 2021 ukumbi wa Silisos.

Diwani kata ya Nyasimo Mhe. Mickness Mahela amehoji kuhusu suala la uwepo wa Mahakama wilayani Busega, akisema kwamba imekuwa kero kubwa kwa wakazi wa Busega wanapotaka kupata huduma ya mahakama, kwani inawalazimu kwenda Wilaya jirani ya Bariadi kupata huduma hiyo.

"Wilaya ya Busega ina takribani miaka tisa kwasasa, hivyo uwepo wa mahakama ni muhimu kwa wananchi wetu" aliongeza Mhe. Bi. Mickness Mahela. Wajumbe wa baraza hilo wamekiri kwamba uwepo wa mahakama ni suala lisilopingika, huku wakidai kwamba wilaya inahitaji mahakama ili kuondoa kero ya wakazi na wananchi wa Busega.

Akitoa ufafanuzi wa suala la uwepo wa mahakama wilayani Busega, mwakilishi kutoka Ofisi ya Mkuu wa wilaya Busega Bw. David Pallangyo anasema kwamba ni suala ambalo Ofisi ya Mkuu wa Wilaya imekua ikifuatilia kwa ukaribu na inaendelea na ufutiliaji. Kwa upande mwingine ameeleza kwamba licha ya watumishi wa mahakama kupangiwa kufanyia kazi zao wakiwa Busega lakini bado wanafanyia kazi zao wilayani Bariadi.

www.busegadc.go.tz
@busegadc busegadc
@busegadistrict halmashauri ya wilaya ya busega

Aidha, hoja ya matengenezo ya magari iliibuliwa na wajumbe huku wakitaka uwepo wa gereji ya halmasuri ili kuwa na ufanisi wa matengenezo ya magari hayo kuliko kupeleka magari hayo kwa Wakala wa Ufundi wa Umeme na utengenezaji wa Magari ya Serikali (TEMESA). Akitoa ufafanuzi wa suala hilo Mkurugenzi Mtendaji Bw. Anderson Kabuko licha ya changamoto ya TEMESA, lakini tayari marekebisho na matengenezo madogo yanafanyika kwa baadhi ya magari na kazi hiyo inafanywa na fundi wa halmashauri.



Picha: Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Busega Mhe. Sundi Muniwe (katikati), Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Busega Mhe. Ng'habi Mojo (wa kwanza kushoto) na Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Busega Bw. Anderson Kabuko wakati wa Kikao cha Baraza la Madiwani Robo ya Tatu.

Suala la stendi ya Wilaya ambayo imeanza kufanya kazi mwanzoni mwa mwezi wa tano mwaka huu, pia limepata wasaa wa kujadiliwa na baraza hilo. Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri ya Wilaya ya Busega Bw. Anderson Kabuko amesema tayari halmashauri imevunja mkataba na mkandarasi wa awali ambae alikuwa akijenga stendi hiyo kutokana na kutofikia ubora wa ujenzi, na tayari utaratibu unafanyika ili kumpata mkandarasi mwingine. Baraza hilo limetaka ujenzi wa wa stendi hiyo uboreshwe hasa njia za kupita magari ili kuondoa usumbufu na kero.

Akiahirisha kikao cha baraza hilo, Mwenyekiti wa halmashauri ya Wilaya ya Busega Mhe. Sundi Muniwe, ametaka kuendelea kwa juhudi ujenzi wa stendi ya Wilaya, na kuagiza kwamba kwasasa hatuhitaji mkandarasi, mhandisi wa ujenzi kwa kushirikiana na Meneja wa TARURA kufanya kazi ya ujenzi kuendelea na ujenzi wa stendi ya Wilaya, Nyashimo. Kwa upande mwingine ameomba viongozi wa mkoa kufuatilia suala la mahakama ili wilaya ya Busega iweze kupata mahakama.

## Ziara ya Kamati ya Siasa Wilaya Busega yatembelea Miradi ya Maendeleo; yaridhika na Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo



Pichani Kamati ya Siasa Wilaya ya Busega ikiwa Ziarani kukagua Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Mkurugrnzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Busega, Bw. Anderson Kabuko akitoa ufafanuzi wa ujenzi wa Madarasa Shule ya Msingi Mirambi mbele ya Kamati hiyo.

Kamati ya Siasa Wilaya ya Busega imetembelea miradi ya maendeleo inayotekelezwa Wilayani Busega. Ziara hiyo iliyoongozwa na Mwenyekiti wa Kamati hiyo Mhe. Daudi Ng'hindi imefanyika kwa siku

www.busegadc.go.tz
@busegadc
busegadc
@busegadistrict
halmashauri ya wilaya ya busega

mbili, kuanzia tarehe 18 hadi 19 Juni, 2021. Katika ziara hiyo Kamati ya Siasa imeweza kutembelea miradi ya sekta ya elimu, maji,



**Pichani ni Kamati ya Siasa ya Wilaya ya Busega ikiwa katika Kituo cha Afya Nassa, Kata ya Nyashimo, ilipofanya Ziara ya kukagua Ujenzi wa Miundombinu Kituoni hapo.**

afya, na kwa sehemu kubwa imeridhishwa na utekelezaji wa miradi hiyo.

**Elimu**

Miradi liyotembelewa katika sekta ya elimu ni mradi wa ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa na ofisi 1 Shule ya Msingi Mirambi kwa gharama ya TZS Milioni 30, ujenzi wa vyumba 3 vya madarasa Shule ya Msingi Mwanangi kwa gharama ya TZS Milioni 60, madarasa yamekamilika na yanatumika, ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa Shule ya Sekondari Nyaruhande kwa gharama ya TZS Milioni 21.3, ujenzi wa maabara Shule ya Sekondari Gininiga kwa gharama ya TZS Milioni 13, ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa Shule ya Msingi Fogofogo na matundu 7 ya vyoo kwa gharama ya TZS Milioni 47.7, ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa Shule ya Sekondari Kabita kwa gharama ya TZS Milioni 40, ujenzi umekamilika, ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa na matundu 7 ya vyoo Shule ya Msingi Itongo kwa gharama ya TZS Milioni 47.7 ujenzi umekalika, ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa na matundu 7 ya vyoo Shule ya Msingi Mwamajashi kwa gharama ya TZS milioni 47.7, ujenzi umekamilika.

**Afya**

Ujenzi wa wodi tatu za wanaume, wanawake na watoto Hospitali ya Wilaya ya Busega, ambapo Serikali imetoa kiasi cha TZS Milioni 500. Ujenzi wa majengo hayo unaendelea. Ujenzi, ukarabati wa vyoo na uwekaji wa miundombinu ya maji Kituo cha Afya kiloleli kwa gharama ya t TZS Milioni 27, ujenzi, ukarabati wa miundombinu ya vyoo vya Watumishi na uwekaji wa miundombinu ya maji Zahanati ya Badugu kwa gharama ya TZS Milioni 20, ujenzi wa vyoo vya wagonjwa na watumishi na uwekaji wa miundombinu ya maji kwa gharama ya TZS Milioni 20 Zahanati ya Ngasamo, ujenzi wa vyoo vya watumishi na uwekaji wa miundombinu ya maji Zahanati ya Shigala kwa gharama ya TZS Milioni 20, ujenzi wa vyoo na uwekaji wa miundombinu ya maji kwa gharama yaTZS Milioni 25, ujenzi wa miundombinu ya vyoo na uwekaji wa miundombinu ya maji Zahanati ya Kijesrishi kwa gharama ya TZS Milioni 20.

**Maji**

Ujenzi mradi wa tanki la maji Mkula wenye thamani ya TZS Bilioni 2.1 ambapo tanki hilo lina ukubwa wa lita 300,000. Ujenzi

www.busegadc.go.tz
@busegadc busegadc
@busegadistrict halmashauri ya wilaya ya busega

unaendelea na mpaka sasa ujenzi umefikia asilimia 60, ukamilikaji wa mradi huu utahudumia watu 16,108 ambapo vituo 33 vitajengwa kwaajili ya huduma ya maji Wakazi wa Mkula, Lutubiga na Kijerishi.



**Picha: Kamati ya Siasa ya Wilaya ya Busega ikiwa katika Mradi wa Ujenzi wa Tanki la Maji Mkula wenye thamani ya TZS Bilioni 2.1. Ujenzi wa Mradi huu Unaendelea.**

Pia kamati hiyo imeweza kutembelea ujenzi wa mradi wa maji Mwamanyili ambao tahamani yake ni TZS Milioni 227.7 ambapo utekelezaji wa mradi huu ni asilimia 45 mpaka sasa. Ujenzi wa tanki wa mradi huo wenye ukubwa wa lita 225,000 umekamilika hatua iliyobaki ni kuanza usambazaji maji kwa watumiaji.

**Miradi Mingine**

Mradi mwingine ambao ulitenmbelewa na ziara hiyo, ni mradi wa ujenzi wa soko la Masanza Kata ya Kiloleli, ambapo kamati ilifika kukagua ujenzi wa choo cha Soko ambacho kimegharimu TZS Milioni 6. Katika ukaguzi wa choo hicho kamati imeagiza Ofisi ya Mkurugenzi kuendelea na jitihada za kuweka miundombinu katika choo hicho ikiwemo maji na umeme ili kuweka mazingira bora pale kitakapoanza kutumika.

Aidha, kamati ya siasa Wilaya ya Busega imeweza kufika katika Vyama vya Msingi vya Ushirika (*AMCOS*), ambapo walitembelea AMCOS ya Bushigwamh'ala iliyopo Kata ya Kalemela na AMCOS ya Kijerishi iliyopo Kata ya Mkula, kukagua na kujionea hali ya ununuzi wa Pamba. Kamati hiyo ikiwa katika AMCOS hizo imeweza kupata taarifa kutoka kwa viongozi lakini pia kusikiliza changamoto wanazokutana nazo, hasa wauzaji wa Pamba ili kuzifanyia kazi.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Busega Bw. Anderson Kabuko amewashukuru wajumbe wa kamati hiyo na kuahidi kutekeleza mambo yote yaliyoelekezwa na kamati hiyo ili kuendelea kuboresha huduma Wilayani Busega kupitia utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo.

Akihitimisha ziara hiyo Mwenyekiti wa Kamati ya Siasa Wilaya ya Busega Mhe. Daudi Ng'hindi, amesema ili kuhakikisha miradi ya maendeleo inatekelezwa kikamilifu ni muhimu kuwa na ushirikiano katika kutekeleza miradi hiyo, na kuzingatia maelekezo yanayotolewa.

www.busegadc.go.tz
@busegadc busegadc
@busegadistrict halmashauri ya wilaya ya busega

## RC David Kafulila Ataka Uvuvi Kuwa Kichocheo cha Maendeleo Busega



Picha: Mkuu wa Mkoa wa Simiyu Mhe. David Kafulila akisalimiana na Viongozi wa Wilaya ya Busega, Alipowasili Busega kuhudhuria Baraza la Madiwani la Kujadili Hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka ulioishia 30 Juni 2020.

Mkuu wa Mkoa wa Simiyu Mhe. David Kafulila ametaka uvuvi kuwa fursa ya kimkakati katika kuchochea maendeleo Wilayani Busega. Ameyasema hayo wakati wa Baraza la Madiwani la Kujadili Hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka ulioishia 30 Juni 2020 Wilayani Busega, lililofanyika tarehe 24 Juni 2021.

Mhe. Kafulila amesema ni wakati sasa umefika kwa Wilaya ya Busega kuhakikisha inafanya mapinduzi makubwa ili kutumia sehemu ya ziwa Viktoria kuongeza tija ya shughuli za uvuvi. "Mnatakiwa kuhakikisha mnatumia fursa ya uvuvi kuleta kasi ya maendeleo, shughuli ya uvuvi iwe miongoni mwa mikakati muhimu ya Wilaya ya Busega", aliongeza Kafulila.

Kwa upande mwingine Mhe. Kafulila amesema kipaumbele cha uvuvi na vipaumbele vingine haviwezi kufanikiwa kama hakutakuwa na usimmamizi na muamko wa wananchi. Amewataka wawakilishi wa wananchi, ambao ni madiwani kusimamia vyema Mipango ya Halmashauri kupitia vikao vya mabaraza."Kuongeza ufugaji wa Samaki kupitia vizimba itaongeza shughuli za uvuvi Wilayani Busega", alisema Kafulila.

Mhe. Kafulila pia ametaka kuimarika kwa usimamizi wa kilimo cha zao la Pamba, kwani Mkoa wa Simiyu unachangia zaidi ya asilimia 55 ya Pamba yote nchini. Amesisistiza kwamba malengo ya Mkoa kwenye uzalishaji wa zao la Pamba kwa msimu ujao ni kufikia tani 500,000, ambapo itasaidia kuongeza mapato ya Halmashauri za Mkoa wa Simiyu.

Mhe. Kafulila amesema kwamba ili kufikia

500,000, ni muhimu kuweka mikakati, ikiwemo kuhakikisha kila mkulima wa zao la Pamba anapatiwa mbolea, hasa mbolea ya Samadi. Kwa upande mwingine Kafulila ametaka kusimamiwa vyema uuzaji wa pamba ili kulinda maslahi ya Wakulima, na kusisitiza kutowaonea haya wote watakaobainika kuhusika na wizi wa ununzi wa Pamba.

Awali, Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Mkoa wa Simiyu Bw. Gwamaka Mwakyosi, amesema Busega imeendelea kupata hati safi, lakini ametaka uzingatiaji wa matumizi bora ya fedha za Serikali ili kuongeza ufanisi wa shughuli mbalimbali.

Akifungua kikao cha Baraza hilo Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Busega Mhe. Sundi Muniwe, kabla ya kumkaribisha mgeni rasmi ambae ni Mkuu wa Mkoa wa Simiyu

www.busegadc.go.tz
@busegadc
busegadc
@busegadistrict
halmashauri ya wilaya ya busega

mhe. David Kafulila, aliweza kumkaribisha Mkuu wa Wilaya ya Busega Mhe. Gabriel Zakaria ili ajitambulishe, kwani ni mara yake ya kwanza kuhudhuria Baraza hilo tangu ateuliwe katika nafasi hiyo.

Mhe. Gabriel Zakaria amesema anajisikia furaha kuhudhuria kikao cha Baraza la Madiwani na kusisitiza kwamba amekuja kuwatumikia Wananchi wa Wilaya ya Busega kwani yupo tayari kushirikiana na viongozi wa Wilaya ya Busega. Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Busega Bw. Anderson Kabuko amesema Ofisi yake itayafanyia kazi maelekezo yote yaliyotolewa na Mkuu wa Mkoa ili kufikia malengo ya Serikali.

## Mbio Maalum za Mwenge wa Uhuru 2021 Wilayani Busega



**Picha: Mkuu wa Wilaya ya Busega Mhe. Gabriel Zakaria akipokea Mwenge wa Uhuru kutoka kwa Mkuu wa Mkoa wa Simiyu Mhe. David Kafulila mara baada ya kupokea Mwenge wa Uhuru kutoka kwa Mkuu wa Mkoa wa Mara Mhe. Alli Hapi katika Viwanja vya Shule ya Sekondari Antony Mtaka tarehe 28 Juni 2021.**







www.busegadc.go.tz
@busegadc
@busegadistrict
busegadc
halmashauri ya wilaya ya busega

## Yaliyojiri Mbio Maalum za Mwenge wa Uhuru 2021 Wilayani Busega

Mbio Maalum za Mwenge wa Uhuru zimepokelewa siku ya tarehe 28 Juni 2021 na kupita katika miradi sita kwaajili ya kuzindua, kuweka jiwe la msingi na kutembelea. Akiupokea Mwenge wa Uhuru, Mkuu wa Wilaya ya Busega Mhe. Gabriel Zakaria amesema Wilaya yake imejipanga kikamilifu kuupokea na kuukimbiza Mwenge wa Uhuru katika miradi yote iliyopangwa.

Kiongozi wa Mbio Maalum za Mwenge wa Uhuru 2021 Luteni Josephine Paul Mwambashi amewapongeza Wananchi wa Wilaya ya Busega kwa kushiriki katika miradi mbalimbali ya maendeleo. “Nawapongeza wananchi kwa kushiriki katika utekelezaji wa miradi mbalimbali, Serikali inatekeleza fedha nyingi za miradi lakini Wananchi mkishiriki kikamilifu katika miradi hiyo lazima tuwapongeze, alisema Luteni Mwambashi.

Aidha, Luteni Mwambashi amesisitiza utunzaji wa nyaraka za miradi mbalimbali ili kuonesha uhalisia wa utekelezaji wa miradi hiyo. Amesema ni vyema nyaraka na vilelezo muhimu viambatane na taarifa za miradi. Aidha, Luteni Mwambashi ameweza kutembelea banda la Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, TEHAMA na kupata maelezo ya baadhi ya mifumo ikiwemo mfumo wa ukusanyaji Mapato ya Serikali na mingineyo.

Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya ya Busega Mhe. Gabriel Zakaria amewashukuru viongozi na Wananchi wa Wilaya ya Busega kwa kuonesha mshikamano katika mapokezi na ushiriki wao katika Mbio Maalum za Mwenge wa Uhuru.

Kauli Mbiu ya Mbio Maalum za Mwenge wa Uhuru 2021***"TEHAMA ni Msingi wa Taifa Endelevu, Itumike kwa Usahihi na Uwajibikaji"***.

Miradi ipatayo sita imeweza kupitiwa na Mbio Maalum za Mwenge wa Uhuru 2021 Wilayani Busega kwaajili ya kuzinduliwa, kuwekwa jiwe la msingi na kutembelewa. Miradi hiyo imejumuisha mradi wa Ujenzi Zahanati ya kijiji cha Mkula wenye thamani ya TZS Milioni 104.3, mradi wa ujenzi wa Hotel ya Sandmark wenye thamani ya TZS Bilioni 2.2, mradi wa Maji Nyashimo wenye thamani ya TZS Bilioni 2.287, Club ya Wapinga Rushwa ambapo mpaka sasa thamani yake TZS 80,000, mradi wa Maabara Sekondari ya Antony Mtaka wenye thamani ya TZS Milioni 58.51 na kutembelea mradi wa kisima cha maji ambao ulizinduliwa na Mbio za Mwenge wa Uhuru mwaka 2019 ili kuangalia maendeleo ya mradi, ambao thamani yake ni TZS Milioni 16.6. Mkuu wa Wilaya ya Busega amekabidhi Mwenge wa Uhuru kwa Mkuu wa Wilaya ya Bariadi leo tarehe 29 Juni 2021, kwaajili ya kuendelea na mbio hizo katika Wilaya zingine za Mkoa wa Simiyu.

www.busegadc.go.tz
@busegadc busegadc
@busegadistrict halmashauri ya wilaya ya busega

## Ziara ya Mkuu wa Mkoa Mhe. David Kafulila Wilayani Busega

Mkuu wa mkoa wa Simiyu Mhe. David Kafulila amefanya ziara ya siku moja wilayani Busega siku ya Tarehe 08 Juni 2021. Katika ziara hiyo Mhe. Kafulila amefanya mkutano wa hadhara na wananchi wa kijiji cha Nyamikoma kilichopo kata ya Kabita. Akiongea na wananchi Mhe. Kafulila amewataka wananchi wa kijiji hicho ambao shughuli zao kubwa ya kiuchumi ni uvuvi kuunda vikundi ambavyo vitawawezesha kupata mikopo kwa kupitia Serikali ili kuongeza tija ya shughuli uvuvi. "Tunahitaji kuwa na umoja katika shughuli zetu, ikiwemo kuunda vikundi ambapo itasaidia vikundi hivyo kupata msaada, ikiwemo mikopo" alisema Mhe. Kafulila. Wakazi wa kijiji cha Nyamikoma wanakabiliwa na changamoto ya kutokuwa na mitaji ya kutosha katika



Pichani ni Mkuu wa Mkoa wa Simiyu Mhe. David Kafulila (katikati), Aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Busega Mhe. Tano Mwera (kushoto), Mkurugenzi Mtendaji halmashauri ya wilaya ya Busega Bw. Anderson Kabuko (kulia) wakati wa ziara ya Mhe. Kafulila Tarehe 08/06/2021 wilayani Busega.

www.busegadc.go.tz
@busegadc
@busegadistrict
busegadc
halmashauri ya wilaya ya busega

shughuli zao za uvuvi, hasa kwa wavuvi wadogo.

Mhe. Kafulila amesema ili kuwa na tija ya uvuvi ni lazima kuboresha shughuli za uvuvi ikiwemo kuwekeza ufugaji wa samaki kwa kutumia vizimba ambavyo kwa tathmini mvuvi ana uwezo wa kupata samaki 1,500 kwa wakati mmoja. Kuhusu suala la soko la samaki, Mhe. Kafulila amesema atafuatilia na kufanya jitihada kwa kuishirikisha Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Halmashauri ili kufanikisha ujenzi wa soko la samaki.
kwa upande mwingine wananchi wa kijiji cha Nyamikoma wameweza kueleza kero zinazowakabili ikiwemo suala la uvamizi wa viboko, na mgogoro wa shamba la kijiji ambalo limevamiwa na watu na kujimilikisha. Mhe. Kafulila amemuagiza Mkuu wa Wilaya kumaliza mgogoro huo. Kuhusu suala la viboko, akitoa ufafanuzi Mkurugenzi Mtendaji amesema Kwamba mara nyingi anapokea malalamiko ya uvamizi wa wanyama na kueleza kwamba huwa wanatoa taarifa kwa vyombo vinavyohusika ikiwemo askari wa wanyapori Bunda (KDU).
Mhe. Kafulila amefanya ziara yake ya kwanza wilayani Busega na kuahidi kwamba atafanya kazi kwa kushirikiana ili kuhakikisha mkoa wa Simiyu unapiga hatua zaidi kimaendeleo. Pamoja na Mhe. Kafulila kufanya mkutano wa hadhara pia ameweza kutembelea baadhi ya miradi ya maendeleo, ikiwemo mradi wa ujenzi wa zahanati kijiji cha Mkula, Ujenzi wa maabara shule ya sekondari Antony Mtaka, na mradi wa maji Nyashimo.



**Pichani: Mkuu wa Mkoa wa Simiyu Mhe. David Kafulila (kulia) alipofika katika Ofisi za Halmashauri ya Wilaya ya Busega na kukaribishwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Busega Bw. Anderson Kabuko (kushoto). Mhe. Kafulila amefanya ziara yake ya kwanza Wilayani Busega tangu ateuliwe kuwa Mkuu wa Mkoa wa Simiyu.**

www.busegadc.go.tz
@busegadc
@busegadistrict
busegadc
halmashauri ya wilaya ya busega

## Busega Yang'ara UMITASHUMTA, UMISETA Yapata Ushindi wa Jumla Ngazi ya Mkoa



Pichani ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Busega Bw. Anderson Kabuko (aliyekaa katikati), Afisa Mipango Wilaya ya Busega Bw. Juma Rahisi (aliyekaa kushoto) na Afisa Michezo Wilaya ya Busega Bi. Macklina Ng'itu (aliyekaa kulia) wakiwa katika picha ya pamoja na Walimu wa Michezo Waliosimamia Vyema Wanafunzi walioshiriki mashindano ya UMISETA NA UMITASHUMTA 2021.

Wilaya ya Busega imeweza kuwa mshindi wa jumla kwenye Mashindano ya Umoja wa Michezo na Taaluma kwa Shule za Msingi Tanzania (UMITASHUMTA) na Umoja wa Michezo na Taaluma kwa Shule za Msingi Tanzania (UMITASHUMTA) na Umoja wa Michezo ya Shule za Sekondari (UMISETA) yaliyofanyika wilayani Maswa kuanzia tarehe 28 Mei hadi juni 12, 2021.

Katika mashindano hayo Wilaya ya Busega imeweza kufanya vizuri katika michezo yote hivyo kuwa mshindi wa jumla kwa mkoa wa simiyu. "nimefurahishwa sana na ushindi huu, kwani mmetuleta heshima kubwa kwa Wilaya ya Busega", hayo yamesemwa na Mkuu wa Wilaya ya Busega Mhe. Tano Mwera wakati wa mapokezi kwa washiriki waliowakilisha vyema Wilaya, mapokezi yaliyofanyika viwanja vya Ofisi ya halmashauri Wilaya ya Busega.

Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri Wilaya ya Busega Ndg. Anderson Kabuko amesema kwamba mafanikio hayo ni jitihada za kila mmoja na amewapongeza wote waliosimamia vyema katika ngazi zote kuhakikisha Busega inafanya vyema ikiwemo walimu. Aidha, ameahidi kutoa vyeti kwa walimu wote waliofanikisha ushindi kwa Wilaya kwani wanastahili sifa na pongezi.

Awali, Mhe. Mwera amempongeza Mkurugenzi Mtendaji na kuomba kuwe na utaratibu wa kutoa zawadi zaidi kwa wanafunzi kwani itasaidia kuwasukuma zaidi katika kujituma na kuitangaza Wilaya ya Busega katika michezo. Aidha, ameeleza kwamba michezo ni ajira hivyo michezo iendelee kuwa moja ya vipaumbele ili kuongeza ajira kwa vijana. Kwa upande mwingine Mhe. Mwera amesema licha ya kufanya vizuri katika michezo ana imani kubwa watafanya vizuri kwenye mitihani ya kitaifa ili Busega iendelee kung'ara.

Kwa upande wake, Afisa Michezo Wilaya ya Busega Bi. Macklina Ng'itu amesema watazidi kuinua michezo, kwani michezo ina fursa nyingi sana kwa vijana ukiachana na ajira pia michezo hutoa fursa za ufadhili wa masomo, hivyo vijana wasisite kungia kwenye michezo mbalimbali.

Aidha, Wilaya ya Busega imefanikiwa kuwa mshindi wa jumla mashindano ya Umoja wa Michezo ya Shule za Sekondari (UMISETA) kwa mkoa wa Simiyu.

www.busegadc.go.tz
@busegadc
busegadc
@busegadistrict
halmashauri ya wilaya ya busega



”.

**Pichani** ni wajumbe wa kamati ya Uchumi, Ujenzi na Mazingira ya halmashauri Wilaya ya Busega, walipofanya ziara ya kukagua eneo la ekari 30 ambazo zinatarajiwa kuuzwa kwa mwekezaji. Kamati hiyo imekagua eneo hilo ambalo litatumika kwa uwekezaji wa kilimo cha umwagiliaji. Mwekezaji anatarajia kununua ekari 50 katika eneo la Nyanza, ambazo zitatumika kwa shughuli za kilimo cha umwagiliaji na uwekezaji wa viwanda.

Kamati hiyo imeridhishwa na mpango wa uwekezaji huo, pia imetaka mchakato wote wa uwekezaji, ufuate kanuni na taratibu za uwekezaji ili kufanikisha uwekezaji wenye tija Wilayani Busega. Kwa upande mwingine kamati hiyo imetaka uzingatiaji na utunzaji wa mazingira kwa mwekezaji yeyote atakayetaka kuwekeza katika eneo hilo na maeneo mengine Wilayani Busega.

Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri Bw. Anderson Kabuko ameitoa hofu kamati hiyo, pamoja na mengineyo pia ameieleza kamati hiyo kwamba, halmashauri ipo kwenye vipaumbele vya uwekezaji ikiwemo uwekezaji wa Kilimo, Uvuvi na Viwanda.